**MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA NA UONGOZI KUJADILI TAARIFA YA ROBO YA KWANZA YA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 NA MAPATO NA MATUMIZI YA MWEZI SEPTEMBA, 2021 KILICHOFANYIKA TAREHE 28/10/2021 KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA MANISPAA YA ILEMELA.**

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA**

1. MSTAHIKI MEYA R.B. MULUNGA - MWENYEKITI
2. ENG. MODEST J. APOLINARY - MKURUGENZI - KATIBU
3. MHE.MANUSURA S. LUSIGALIYE - NAIBU MEYA - MJUMBE
4. MHE. DKT. ANGELINE S.L. MABULA- MBUNGE - MJUMBE
5. MHE. SWILA D. SWILA - MJUMBE
6. MHE. ANTHONY A. NGINILA - MJUMBE
7. MHE. SARAH R. LISSO - MJUMBE
8. MHE. GODLISTEN KISANGA - MJUMBE
9. MHE. KURUTHUM S. ABDALLAH - MJUMBE
10. MHE. ABDULRAHMAN SIMBA - MJUMBE

**WATAALAM WALIOHUDHURIA**

1. BW. BENSON P. MIHAYO - AFISA UTUMISHI MKUU
2. BI. BRIGITA MSANGYA - K/AFISA MIPANGO MIJI
3. ENG. JUMA T. KING'OLA - KAIMU MHANDISI MANISPAA
4. BW. PATRICK M. MUHERE - MWANASHERIA
5. BW. MARCO JOSEPH - AFISA USAFIRISHAJI
6. BW. DICKSON CHRISTOPHER - K/MRATIBU VIHATARISHI
7. BW. ALTO MBIKIYE - AFISA UCHAGUZI
8. BW. SITTA SINGIBALA - AFISA MAENDELEO YA JAMII
9. BI. BERTHA A. GEORGE - AFISA MASOKO
10. BW. JAMES DALASIA - MWEKA HAZINA
11. BW. WITNESS MUGYABUSO - K/AFISA ELIMU MSINGI
12. BW. FUNDIKIRA K. JAMES - KATIBU TSC
13. BI. SUZANE TILUMANYWA - K/AFISA TARAFA
14. BW. MVANO KARUMBETE - AFISA UGAVI
15. BW. ISACK D. TANGUYE - K/AFISA HABARI MANISPAA
16. BW. ABDUL MBAGA - MKAGUZI WA NDANI
17. BW. EMMANUEL C. MALIMA - AFISA ELIMU SEKONDARI
18. BI. ELIZABETH SWAGI - AFISA BIASHARA
19. BW. MUSSA MUKONGA - K/AFISA MIFUGO NA UVUVI
20. BW. MOPHEN G. MWAKAJONGA - MCHUMI WA MANISPAA
21. BW. HAMISI MLEWA - AFISA AFYA
22. BI. NEEMA SEMWAIKO - AFISA KILIMO & UMWAG.
23. BW. FRANK NGITAOH - MRATIBU WA TASAF
24. BW. PETRO YOHANA - K/AFISA USAF. NA MAZ.
25. BW. NICOLAUS KAWANA - AFISA MAPATO
26. BW. DANIEL SAGWA - MHASIBU
27. BW. ALBERT KAMUHABWA - AFISA TEHAMA

28. DR. SAMSON M. CHARLES - MGANGA MKUU
29. BW. WILLIE T. KISANJI - MRATIBU WA UKIMWI
30. BI. THERESIA N. CHRISANT - AFISA USHIRIKA
31. BW. WILFRED MAGIGE - MTHIBITI UBORA

**SEKRETARIETI**

1. BI. RACHEL E. LUBUBU - MRATIBU WA VIKAO
2. BI. ESTER J. MWANGOTA - AFISA TAWALA
3. BW. LUGEMBE S. JEREMIAH - MWANDISHI WA VIKAO
4. BW. SHILINDE MALYAGILI - MWANDISHI WA VIKAO
5. BI. WINFRIDA B. MAGEMBE - MWANDISHI WA VIKAO

**AGENDA ZA KIKAO**

1. Kufungua kikao
2. Kuthibitisha Agenda.
3. Kusoma na kuthibitisha Muhtasari wa kikao cha tarehe 28/09/2021 na tarehe 29/09/2021.
4. Yatokanayo na Muhtasari wa kikao cha tarehe 28/09/2021.
5. Kujadili taarifa ya Mapato na Matumizi ya Mwezi Septemba, 2021.
6. Kupokea na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa shughuli zilizo chini ya Kamati ya Fedha na Uongozi kwa Robo ya kwanza, 2021/2022.
7. Taarifa ya Ziara ya Kamati ya Fedha na Uongozi kwa Robo ya kwanza 2021/2022 iliyofanyika tarehe 22/10/2021.
8. Taarifa ya mapokezi ya fedha Tshs. 1,940,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa katika Shule za Sekondari.
9. Ombi la kuondoa mashine 165 za kielektroniki (POS) zilizoharibika.
10. Mapendekezo ya punguzo la kodi ya vyumba/meza katika masoko ya Buzuruga na Sabasaba nafaka
11. Ombi la Waheshimiwa Madiwani kupatiwa viwanja katika mradi wa viwanja wa East Buswelu
12. Kufunga kikao.

**IMC/FINANCE/AG.NA. 22/3/OKTOBA/2021: KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti aliwakaribisha Wajumbe na Wataalam na kuwaomba kushiriki kikamilifu katika kujadili agenda zilizokuwa mezani kisha alifungua kikao saa 02:34 Asubuhi.

**IMC/FINANCE/AG.NA.23/3/OKTOBA/2021: KUTHIBITISHA AGENDA**

Katibu wa kikao aliwasilisha jumla ya agenda 9 zilizokuwa mezani, agenda 3 ziliongezeka ambazo ni ombi la kuondoa mashine za POS 165 zilizoharibika na Mapendekezo ya punguzo la kodi ya vyumba/ Meza katika masoko ya Buzuruga na Sabasaba pamoja na Ombi la Waheshimiwa Madiwani kupatiwa viwanja katika mradi wa Viwanja wa East Buswelu na kufanya jumla ya agenda kuwa 12. Wajumbe walizipokea na kukubaliana ziweze kujadiliwa kisha kikao kiliendelea.

kwa ajili ya ujenzi wa choo katika soko la Nyambiti zitolewe ili kukamilisha ujenzi wa choo hicho ambapo maombi hayo yalizingatiwa.

Kuhusu fedha kwa ajili ya ukarabati wa taa za barabarani, ufafanuzi ulitolewa kuwa Bajeti iliyotengwa kwa ajili ya taa za barabarani ni Tshs. 90,000,000.00 ambazo zitatumika kwa ajili ya kufanya ukarabati na kununua taa mpya. Wajumbe walisistiza kuwa taa za barabarani ni vyema zikafanyiwa ukarabati kwa sababu taa nyingi hususani katika barabara ya Nyasaka - Buzuruga zimeharibika ambapo Menejimenti iliahidi kufanyia kazi suala hilo na kasha agenda hiyo ilifungwa.

**IMC/FINANCE/AG.NA.29/3/OKTOBA/2021: TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA TSHS. 1,940,000,000.00 KWA AJILI YA UJENZI WA VYUMBA VYA MADARASA KATIKA SHULE ZA SEKONDARI.**

Taarifa hiyo iliwasilishwa kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela imepokea kiasi cha Tshs. 1,940,000,000.00 kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa vipatavyo 97 katika shule mbalimbali za sekondari. Sambamba na taarifa hiyo, Menejimenti iliwasilisha pia mpango wa usimamizi wa utekelezaji wa ujenzi huo ambapo ilielezwa kuwa kutakuwa na fomu maalum ambayo itakuwa ikitumika katika utoaji wa taarifa ya maendeleo ya ujenzi kwa kila siku na taarifa hizo zitatakiwa kuthibitishwa na wahusika tofauti wakiwemo viongozi wa Chama Tawala wa Kata/Tawi.

Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa, wajumbe waliipokea na kufanya majadiliano kama ifuatavyo:-

Wajumbe waliishukuru Ofisi ya Rais-TAMISEMI kwa kuleta fedha hizo kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa na walitaka kufahamu kama fedha hizo ni kwa ajili ya ukamilishaji au kuanzisha ujenzi mpya. Maelezo yalitolewa kuwa fedha hizo ni kwa ajili ya kujenga vyumba vipya vya madarasa pamoja na kununua madawati.

Aidha wajumbe walitaka kufahamu kwa nini mgao wa fedha hizo upo tofauti ambapo maelezo yalitolewa kuwa fedha hizo zimetolewa kutokana na uhitaji wa kila shule. Vilevile wajumbe walionesha wasiwasi kuwa walimu huenda wasiweze kusimamia vizuri matumizi ya fedha hizo. Ushauri pia ulitolewa kuwa Makatibu wa CCM Kata na Tawi wakague tu utekelezaji wa kazi lakini siyo kukagua vifaa vya ujenzi ili kuondoa mgogoro unaoweza kutokea ambapo madiwani waliahidi kutoa ushirikiano wa kutosha ili kuhakikisha fedha hizo zinatumika ipasavyo.

Aidha ufafanuzi ulitolewa kuwa waliotajwa kwenye fomu kazi yao ni kukagua utekelezaji wa ujenzi na siyo kuingilia majukumu ya Kamati ya ujenzi na wahusika hao hawatakuwa na malipo kwa mujibu wa mwongozo lakini Menejimenti ilitoa maelezo kuwa itatumia fedha za mapato ya ndani angalau kuwawezesha kidogo wahusika hao ili waweze kutekeleza kazi hiyo kikamilifu.

Kuhusu ujenzi wa maabara katika Shule mpya ya Nyamhongolo, taarifa ilitolewa kuwa mahitaji katika ujenzi wa Shule hiyo ni matofali hivyo wajumbe waliomba Menejimenti isaidie kupatikana kwa matofali kwa ajili ya ujenzi wa maabara hiyo ambapo maelezo yalitolewa kuwa Shule mpya hazipo kwenye mgao wa fedha hizo.

Wajumbe walisisitiza kuwa lengo la kujengwa kwa Shule mpya ni kuwapunguzia wanafunzi umbali wa kutembea kwenda shule, hivyo shule hizo zikamilishwe mapema ili kuwatia moyo wananchi waliojitolea kujenga miundombinu ya Shule hizo.

Wajumbe walishauri ujenzi wa vyumba vya madarasa kutokana na fedha iliyoletwa utumie matofali kutoka kwenye mradi wa Halmashauri ili kulinda ubora wa kazi na menejimenti iliahidi kulizingatia hilo kasha agenda hiyo ilifungwa.

**IMC/FINANCE/AG.NA.30/3/OKTOBA/2021: OMBI LA KUONDOA MASHINE 165 ZA KIELEKTRONIKI (POS) ZILIZOHARIBIKA**

Ombi la kuondoa mashine 165 za kielektroniki zilizoharibika liliwasilishwa kuwa kwa mujibu wa kipengele namba 45 (1) cha Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009, mali chakavu zitatambuliwa na kuondolewa baada ya kupata kibali cha Kamati ya Fedha na hivyo idadi ya Mashine chakavu 165 ambazo zilinunuliwa kati ya Mwaka wa Fedha 2015/2016 hadi 2020/2021 zilitakiwa kuondolewa.

Baada ya ombi hilo kuwasilishwa na kupokelewa, wajumbe waliruhusu POS hizo ziondolewe kisha agenda ilifungwa.

**IMC/FINANCE/AG.NA.31/3/OKTOBA/2021: MAPENDEKEZO YA PUNGUZO LA KODI YA VYUMBA/MEZA KATIKA MASOKO YA BUZURUGA NA SABASABA NAFAKA**

Taarifa tajwa hapo juu iliwasilishwa kuwa msingi wa kuwasilisha mapendekezo hayo ni agizo alilolitoa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mheshimiwa Samia Suluhu Hassan wakati wa ziara yake jijini Mwanza tarehe 8/9/2021 na pia malalamiko ya wafanyabiashara wa soko la Sabasaba kupitia barua yao kwa Mkurugenzi wa Manispaa ya tarehe 26/09/2021.

Kwa soko la Buzuruga, Menejimenti ilipendekeza kupunguza bei kutoka Tshs. 200,000.00 kwa mwezi hadi Tshs. 180,000.00 kwa vyumba vya mbele na kutoka Tshs 100,000.00 kwa mwezi hadi Tshs. 80,000.00 kwa vyumba vya ndani. Kwa upande wa Meza Menejimenti ilipendekeza waendelee kulipa kiwango hicho hicho cha Tshs. 9,000.00 kwa mwezi.

**Azimio:** Idara ya Mipango Miji waandae andiko kwa ajili ya maombi ya waheshimiwa madiwani kupatiwa viwanja kisha wawasilishe katika kikao kijacho.

**IMC/FINANCE/AG.NA.33/3/OKTOBA/2021: KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe pamoja na wataalam kwa ushiriki wao katika agenda zilizokuwa mezani na kusisitiza suala la kudhibiti wamachinga kurejea kwenye maeneo yasiyo rasmi waliyoondolewa lifanyiwe kazi kwa sababu tayari wameanza kurejea tena kwenye maeneo hayo na alisisitiza kila mmoja kutimiza wajibu katika eneo lake kisha alifunga kikao saa 10:48 asubuhi.

..........................................................
**SAINI YA KATIBU WA KIKAO**

..........................................................
**SAINI YA MWENYEKITI WA KIKAO**

**TAREHE YA KUTHIBITISHWA MUHTASARI**......19/11/2021......